FUNZO LA 13

1. Ni nini Mungu alichofanya baada ya Adamu na Hawa kutomtii?
-Baada ya Adamu na Hawa kutomtii Mungu, Mungu alimuita Adamu.

2. Je, Mungu alimuita Adamu kwa sababu hakujua alikokuwa Adamu?
-La.
-Mungu anajua kila kitu.
-Mungu anaona kila kitu.

3. Kwa nini Mungu alimuita Adamu?
-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akiri dhambi zake.
-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akubali kuwa hakumtii Mungu.
-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akubali kuwa alimsikiliza Shetani.

4. Je, Mungu alimwadhibu vipi nyoka?
-Nyoka lazima sasa atambae kwa tumbo lake.

5. Mungu alimwadhibu vipi Hawa?
-Hawa angezaa watoto kwa uchungu mwingi.

6. Je, Mungu alimwadhibu vipi Adamu?
-Adamu atalima ardhi kwa jasho jingi, na apate mahindi machache.
-Mungu alilaani ardhi yote.



7. Ni ishara gani zaonyesha kuwa Mungu amelaani ardhi?
-Kuna miiba na magugu mengi.
-Kuna viangazi vingi na gharika nyingi.
-Kuna mimea na nyoka wengi wenye sumu.
-Wanyama wanawauma wanadamu.
-Watu lazima wafanye kazi sana.
-Watu wanakuwa wagonjwa.
-Watu wanakufa.

8. Muda mfupi baada ya Mungu kuwaadhibu Adamu na Hawa, Mungu aliahidi kufanya nini?
-Muda mfupi baada ya Mungu kuwaadhibu Adamu na Hawa, Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi.

9. Mwokozi angefanya nini?
-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za dhambi.
-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za kifo.
-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za Shetani.

10. Mwokozi angekuwa nani?
-Mwokozi angekuwa mwana wa bikira.

11. Kwa nini Mungu aliahidi kutuma Mwokozi?
-Kwa sababu Mungu anawapenda watu wote sana.

12. Je, Adamu na Hawa walistahili upendo wa Mungu?
-La. Kutokutii kwao kulistahili kifo cha milele.

-Adamu na Hawa walifanya nini baada ya kutomtii Mungu?
-Walijitengenezea mavazi kutoka kwa majani.

-Kwa nini Adamu na Hawa walijitegenezea mavazi kutoka kwa majani?
-Kwa sababu walitaka kuficha dhambi yao.

-Je, mtu anaweza kuficha dhambi yake kutoka kwa Mungu?
-La.

-Hakuna anayeweza kuficha dhambi yake kutoka kwa Mungu.

-Lakini Mungu alikataa mavazi ya majani ambayo Adamu na Hawa walitengeneza.

-Kwa nini Mungu alikataa mavazi ya majani ambayo Adamu na Hawa walitengeneza?

-Je, Mungu hapendi majani?
-La.

-Mungu ndiye aliyeumba majani.

-Kwa nini Mungu alikataa mavazi ya majani amabayo Adamu na Hawa walitengeneza?

-Mungu alitaka kuwafundisha Adamu na Hawa kuwa hakuna chochote wangefanya ili awakubali.

-Je, tunawezajifanya kukubalika kwa Mungu kupitia mavazi



tunayovaa?
-La.

-Je, tunawezajifanya kukubalika kwa Mungu kupitia kazi tunayofanya?
-La.

-Mungu hatawakubali wale wanaofuata njia zao.
-Mungu hatawakubali wale wanaochagua njia zao.

-Mungu anataka tufuate njia ya Mungu pekee.
-Mungu anataka tuchague njia ya Mungu pekee.

-Ni nani pekee aliyeweza kufanya Adamu na Hawa wakubalike kwa Mungu?
-Mungu.

-Je, Mungu aliwafinyia nini Adamu na Hawa?

Tusome Mwanzo 3:21

21-Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.

-Mungu aliwafanyia mavazi ya ngozi ya mnyama.

-Je, Mungu alipata wapi ngozi ya mnyama?
-Mungu aliwaua wanyama na kutoa ngozi zao.

-Kwa nini Mungu aliwaua wanayama ili kuwafanyia Adamu na

Hawa mavazi?

-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa.

-Je, Mungu alikuwa akiwafundisha nini Adamu na Hawa?

-Kwamba kutokutii kunaleta kifo.
-Kwamba dhambi inaleta kifo.
-Kwamba adhabu ya dhambi ni kifo.

-Kifo cha kwanza cha kimwili duniani ni pale Mungu alipowaua wanyama.

-Hata kama kutokutii kwa Adamu na Hawa kulistahili kifo, Mungu aliwatengenezea mavazi.

-Kwa nini Mungu aliwatengenezea Adamu na Hawa mavazi?
-Kwa sababu Mungu aliwapenda Adamu na Hawa.

-Adamu na Hawa hawakujivalisha mavazi.
-Ni Mungu aliyewavalisha Adamu na Hawa hayo mavazi.

-Kwa nini Mungu hakuwakubalia Adamu na Hawa kujivalisha hayo mavazi?

-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa kuwa ni Mungu anayewafunika watu.

-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa kuwa hatawakubali wale wanaofuata njia yao.



-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa kuwa hatawakubali wale wanaochagua njia yao.

-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa kufuata njia ya Mungu pekee.

-Mungu alikuwa akiwafundisha Adamu na Hawa kuchagua njia ya Mungu pekee.

-Je, Mungu alifanya nini baada ya kuwavalisha Adamu na Hawa mavazi?

Tusome Mwanzo 3:22-23

22-Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele;
23- kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu walikuwa wakizungumza kuhusu Adamu na Hawa.

-Mwanzoni, Adamu na Hawa walijua mema pekee.
-Sasa, Adamu na Hawa walijua dhambi.

-Mwanzoni, Adamu na Hawa walijua kutii pekee.
-Sasa, Adamu na Hawa walijua kutokutii.

-Mwanzoni, Adamu na Hawa hawakujua aibu.
-Sasa, Adamu na Hawa walijua aibu.

-Mwanzoni, Adamu na Hawa walijua tu uzima.
-Sasa, Adamu na Hwa walijua kifo.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi, Mungu aliwaondoa kutoka katika Bustani ya Edeni.

Tusome Mwanzo 3:24

24-Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima.

-Je, Mungu alifanya nini ili Adamu na Hawa wasirejee katika Bustani ya Edeni?

-Mungu aliwaweka malaika waitwao Makerubi na upanga wa moto katika mlango wa Bustani ya Edeni.

-Je, kwa nini Mungu alifanya hivyo?

-Mungu hakutaka Adamu na Hawa warejee katika Bustani ya Edeni.

-Je, kwa nini Mungu hakutaka Adamu na Hawa warejee katika Bustani ya Edeni?

-Kwa sababu Adamu na Hawa hawakumtii Mungu na walitenda



dhambi.

-Je, Adamu na Hawa walikufa?
-Ndiyo.

-Je, Adamu na Hawa walikufa vipi?

-Adamu na Hawa walitenganishwa na Mungu.
-Adamu na Hawa walitenganishwa na Mungu aliyewapa uzima.

-Adamu na Hawa hawangeweza kuwa na Mungu tena.
-Adamu na Hawa hawangeweza kuishi na Mungu.

-Iliwabidi Adamu na Hawa kuishi katika kutengana na Mungu.

-Mungu ni mtakatifu.
-Mungu hawezi ishi na dhambi.
-Adhabu ya Mungu kwa dhambi ni kifo.

-Adamu na Hawa ni baba na mama ya watu wote.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walikufa, watu wote walikufa.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenganishwa na Mungu, watu wote walitenganishwa na Mungu.

-Mungu ni mtakatifu.
-Mungu hawezi ishi na dhambi.

-Adhabu ya Mungu kwa dhambi ni kifo.